


# KATIBU WA

## UWAKILI KANISANI

Mwongozo huu umekusudiwa kumsaidia mtu yeyote yule kujua jinsi katibu wa uwakili kanisani anavyopaswa kufanya kazi. Hapa kuna vidokezo vichache vinavyohusu: majukumu, kazi, na shughuli anazopaswa kusimamia katibu wa uwakili baada ya kuchaguliwa kuwa kiongozi katika kanisa mahalia.

*North East Tanzania Conference*
Pr. Almodad Amos
+255 718 834 621
modaofpeace@gmail.com

## Utangulizi

Katibu wa uwakili wa kanisa mahalia anayo kazi ya muhimu sana ya kuwa muelimishaji na muweka mipango ya uwakili kanisani. Akiwa kama mjumbe wa baraza la kanisa anashirikiana na mchungaji pamoja na wanabaraza wengine katika kuweka mkakati kazi wa kanisa utakaotimiza utume wa kanisa. Lakini pia hushiriki kupangilia na kusimamia shughuli ya utengenezaji wa mahubiri, program mbalimabli na shughuli za uwakili kwa ujumla kwa mwaka mzima au kipindi kilichokusudiwa. Yeye ndiye kiunganishi kati ya kiongozi wa uwakili konferensi na kanisa mahalia.

## Idara ya Uwakili

Asili ya kazi ya idara ya uwakili iko katika kuwatia moyo waumini kutumia vizuri vitu ambavyo Mungu amewapa, ikiwemo, uwezo, talanta, muda, miili, na hata mali pia. Kanisa mahalia linawajibika kwa ujumla kwa jinsi linavyosimamia vitu walivyopewa waumini, linasimamia malezi ya kiuwakili na kuwaongoza watu katika kuuelewa uwakili ktk Nyanja zote za maisha ya mwanadamu. Tukiutazama uwakili kwa ujumla wake, ndio mzizi wa utume na goli/dhumuni la uanafunzi wa kweli.

Yesu alitumia muda wake mwingi akizungumzia mali na vitu anavyomiliki mwanadamu katika maisha ya kawaida. Alielewa kwamba wasikilazaji wake wasingezielewa vizuri kanuni za ufalme wake mpaka kwanza wameelewa mahusiano yao ya ki-uwakili kwa Mungu wao.

> Kama mawakili, tumeumbwa kwa mfano wa Mungu, ili tuiaksi tabia yake na kuyatenda makusudi yake. Tunapotambua kwamba kila kitu ni mali ya Mungu, tunaweza kujifunza kusimamia kile ambacho tumekabidhiwa kukisimamia kwa mapenzi na mpango wa mbingu.

## Kujipanga na kujiandaa kwa Kazi ya Huduma ya Uwakili

Kwa bahati mbaya sana, katika makanisa yaliyomengi leo hii, shughuli za uwakili na kuweka mipango ya mwaka hufanyika katika namna ambayo si nzuri na yenye kuvutia. Makanisa mengine yanakua na kamati za fedha tu, ambazo huwa na kazi rahisi sana kupita kiasi na ambayo inahusiana na kuifanya bajeti ya kanisa ipitishwe tu, basi. Mabaraza ya kanisa saa nyingine yanalemewa sana na mzingo wa agenda za shughuli nyignine mpaka yanasahau kuweka tamko la utume wa kanisa mahalia na kulisimamia ipasavyo kuanzia kwenye mkakatikazi mpaka kwenye kuweka malengo ya muda mrefu.

Ikiwa tayari kanisa lako mahalia limeweka tamko lake la utume mahali pake na limetathmini changamoto zake na kuweka malengo yake, unamahali pazuri kabisa pa kuweza kuanzia kazi. Ikiwa sivyo, utahitaji kuwa na timu ya watu waliojitoa kikamilifu ambao wanauwezo wa kupangilia na kuweka mikakati; watu ambao wako tayari kutumia muda wao na juhudi zao kusimika tamko la utume wa kanisa mahalia na kuendeleza mipango ya kutimiza utume wa kanisa. Watu hawa kwa kawaida watafanya kazi kama kamati ndogo ya baraza la kanisa na wataleta mapendekezo yao kwa baraza la kanisa.

Katika makanisa madogo, baraza la kanisa watatakiwa kuchukua jukumu hili. Huu mkakati kazi utakaowekwa ni muhimu sana kwa kuwa hauwezi kwa namna yoyote ile ukatenganishwa na bajeti ya kanisa. Viongozi wote na maidara yote wanatakiwa kuwa na muundo wa mpango huu. Ili kufanikiwa, mkakati utatakiwa kuwavutia washiriki na kupata kuungwa mkono na kanisa.

## Kuweka Mkakati wa Bajeti ya Kanisa

Mara tu viongozi wapya wa maidara wanapochaguliwa kanisani, mchakato wa kuweka mpango kazi au mkakati kazi huanza bila kuchelewa. (ikiwezekana miezi miwili au mwezi mmoja kabla ya kuuanza mwaka wa uongozi:

1. **Tengeneza au hakikisha kwamba kuna utume wa kanisa mahalia unaoendana na mazingira ya kanisa lako na kanisa ulimwenguni**. Kumbuka kwamba kauli mbiu ya utume wa kanisa mahalia, inajibu maswali yafuatayo: sisi ni akina nani? tunaamini nini na kufundisha nini? Makusudi yetu ni nini?

2. **Lipime kanisa kwa jinsi livyojishughulisha na kuutimiza utume wake kwa sasa.** Hapa utajihoji maswali haya matatu:

   **Kwa habari ya mambo ya kiroho**: je, kanisa lako linaweka mipango madhubuti ya mwaka kwa ajili ya watu kukua kiroho na kupata malezi ya kiroho? Je, tunafundisha juu ya watu kuzitambua karama za roho na kuzitumia karama hizo vizuri kanisani? Je, tunayo kamati inayohusika na huduma ya maombi, ambayo ni hai?

   **Kwa habari ya kuwashughulisha washiriki**: Je, tunatumia karama za waumini kanisani mara kwa mara au tunatumia vyeo vya viongozi waliochaguliwa tu katika kanisa? Je, tunawaalika washiriki kutoa maoni yao na mawazo yao katika kuunda na kupangilia bajeti ya kanisa? Je, maidara yanatilia maanani utume wa kanisa na uinjilisti, au malezi ya kanisa katika shughuli za kila idara?

   **Vyanzo vya mapato ya fedha**: utoaji wa zaka umeongezeka kwa asilimia ngapi hapo kanisani kwa muda wa mwaka mzima? Je, uwiano wa watu wanohudhuria kanisani na wale wanaotoa zaka na sadaka kwa ujumla uko jinsi gani? Je, matoleo ya sadaka yamongezeka kwa asilimia ngapi kwa mwaka mzima kwa ajili ya bajeti ya kanisa na sadaka ya konferensi ulimwenguni kote?
3. **Tambua na weka vipaumbele kwa kila changamoto** iliyojitokeza katika tathmini uliyoifanya katika kulipima kanisa lako. Wahusishe washiriki baadhi katika kupitia upya na kuutazama tena utume wa kanisa mahalia; na katika kuziangalia changamoto zinazolikabili kanisa kwa sasa. Hatua hizi zitachukua sana muda lakini zitasaidia kukusanya maelezo ya kutosha katika kutambua changamoto zinazolikabili kanisa. Pia utakua ukijenga msingi wa kuungwa mkono na kanisa katika malengo yatakayowekwa.
4. **Weka hatua mbalimbali za utukelezaji wa mkpango kazi**. Hatua hii huhusika sana na mpango kazi katika kila idara husika, utakavyoendana na utume wa kanisa. Badala ya kujikita sana katika orodha ya gharama za vitu, katika hatua za utekelezaji tunaangalia sana jinsi idara inavyowagusa watu. Hii itahusika sana na kusudi la kanisa na kile kinachopaswa kukamilishwa n a watu wa Mungu na pia kuwa baraka kwa watu wa Mungu.

5. **Bajeti ielekeze kwenye utume wa kanisa**. Kaulimbiu ya utume wa kanisa, mpango kazi wa idara na vipaumbele vilivyotokana na changamoto, vinatakiwa kuwekwa kama utangulizi katika bajeti ya kanisa. Hii itatumika kulikumbusha kanisa kwamba bajeti yake ipo ili tu kutimiza utume wa kanisa.

   Katika mpango kazi wa kila idara, bajeti inagawanyika kulingana na utume wa idara na mahitaji ya kanisa mahalia. Kila idara inakua na mipango yake, shughuli zake, na program mbalimbali ambazo zimejengwa juu ya kutimiza utume wa kanisa. Kila kitakachofanyika kinatakiwa kuonyesha jinsi kitakavyosaidia katika kutimiza utume wa kanisa mahalia. Jambo hili linapoeleweka vizuri kabisa, washiriki wanaweza kuona tofauti kati ya kutoa kwa ajili ya "bajeti ya kanisa" na kutoa ili kulisaidia kanisa kutimiza utume wa kanisa kwa ujumla.

   Wakati sampuli hii ya bajeti ya kanisa inapokua imepitishwa na kamati ya mipango/fedha, inaletwa kwa baraza la kanisa ili iweze kupitishwa, na kisha pitishwa kama mpango kazi mkuu wa kanisa na halmashauri kuu ya kanisa. Mara nyingi katibu wa uwakili (ambaye ndiye anapaswa kuwa mwenyekiti wa kamati ya mipango/fedha) anauleta mpango kazi huu, akisaidiwa na mchungaji na/au wazee wa kanisa. Lengo kuu la kutumia mlolongo huu mrefu ni kutafuta kuungwa mkono na washiriki, kwa wingi na kwa kadri inavyowezekana.

6. **Simamia kwa dhati mpango kazi uliowekwa**. Utekelezaji wa makini sana wa bajeti iliyowekwa unahitajika sana ili kanisa liweze kukua na kufikia malengo yake. Taarifa mbalimbali za maendeleo ya kazi zinatakiwa kutolewa mara kwa mara kwa mwaka mzima. Ari ya washiriki kujitoa itaongezeka na matoleo yataongezeka pia ikiwa tutafuata miongozo bora ya uwekaji wa mkakati kazi na kuusimamia vizuri.

   Inashauriwa kwamba, kila robo tuwe na tathmini ya mahali ambapo tumefikia katika utume uliowekwa, changamoto tulizoziona mwanzoni mwa mwaka na juu ya melengo tuliyojiwekea kwa mwaka tunaokuanao. Taarifa hizo ni vizuri ziletwe kwa waumini kanisani zikiwa zimetazamwa kwa makini na baraza ili kanisa lishiriki katika kulishauri baraza.

7. **Kamati ya mipango/bajeti pia itasimamia** mambo yafuatayo kwa makini sana:
   a. *Kuhakikisha kwamba bajeti ya kanisa imetumika kulingana na mpango kazi.*
   b. *Kutoa mapendekezo maalum kwa baraza la kanisa pale mahitaji muhimu ambayo hayakua katika mpango yanapojitokeza.*
   c. *Kuichunguza taarifa ya uwakili kwa vipindi flani vya muda na kutoa taarifa kwa baraza na kisha baraza kuileta kwa kanisa zima.*
8. **Piatia tena kila hatua** ili kujiridhisha na kufanya marekebisho kadhaa: kuwa na mikakati ya kipindi flani cha wakati ambayo inaendana na bajeti ya kanisa ni moja kati ya njia za kuongeza ufanisi wa mafanikio katika kanisa mahalia.

Udhaifu mkubwa ambao uko katikak makanisa yaliyo mengi ni kusubiri sana na kuchelewa sana kuweka na kuanza kusimamia mkakati kazi na hatua zake. Hapa kuna maswali muhimu ya kujihoji ili kutathmini hatua za kuweka mkakati kazi na bajeti kwa ujumla:

- *Ni lini maafisa wa kanisa wanatakiwa kuchaguliwa (viongozi wa kanisa)?*
- *Ni lini hasa tunatakiwa kuupokea mpango kazi wa kila idara kanisani kutoka kwa viongozi wa maidara hayo?*
- *Ni lini hasa mpango kazi na bajeti vinatakiwa kupitishwa na kuanza kazi mara moja?*

## MAFUNZO YA ELIMU YA UWAKULI

Njia za kutumia katika kuwaelimisha waumini kanisani zitatofautiana kulingana na hitaji la kanisa mahalia. Hata hivyo njia zifuatazo zinaweza kutumiaka:

1. Kuwa na mahubiri ya msisitizo juu ya uwakili
2. Kupangilia kwa makini masomo ya matoleo kabla ya muda wa matoleo
3. Shuhuda za watu ambao wanauzoefu wa mibaraka iliyotokana na uaminifu katika uwakili
4. Kufundisha kwa kutumia madarasa maalum, semina na mafundisho ya Biblia
5. Kutumia vipeperushi na majarida au machapisho.
6. Semina juu ya matumizi binafsi ya pesa, na matumizi ya familia pia
7. Kufuata mkakati wa konferensi juu ya uwakili
8. Kushiriki katika majuma ya uamsho ya uwakili
9. Kuwafunza na kuwalea waumini wapya pamoja na watoto katika maswala ya uwakili.
10. Kiongozi kuwa mfano bora katika matoleo
11. Kutengeneza vyombo (masanduku) makubwa na mazuri kwa ajili ya matoleo
12. Kutembelea mtu mmoja mmoja na kuwatia moyo; lakini pia kusikia changamoto za kiuwakili kutoka kwao

**Mtu na Uwakili**

Hii ni program ya kumtembelea mshiriki mmoja mmoja mahali alipo na kuwasiliana naye uso kwa uso kwa kusudi la kuendelea kumtia moyo kujitoa kikamilifu. Kusudi la matembembezi haya ni:

- Kuitazama kaulimbiu ya kanisa pamoja na mshiriki, kuona changamoto, malelngo na mipango ya kanisa.
- Kuona jinsi bajeti ya kanisa inavyohusiana na bajeti ya kanisa, changamoto za kanisa na malengo ya kanisa kwa mwaka husika.
- kuwaalika washiriki kushiriki katika kukamilisha malengo hayo
- kuomba na wanafamiliana washiriki.

Kuweka mpango kazi na kusimamia utekelezaji, ni mambo ya msingi sana katika kuleta mafanikio ya kanisa. Wapatie waumini na washiriki kaulimbiu ya utume, changamoto na malengo ya kanisa pamoja na bajeti ya kanisa iliyokusudiwa

Kwa umakini mkubwa pawe na watu watakaoshiriki katika kutembelea washiriki. ni vema kabisa ikiwa watafanya utembeleaji wawe katika makundi ya watu wawili wawili. Lengo ni kumtembelea kila mshiriki katika kipindi cha juma/majuma flani yaliyokusudiwa na kuwa na mpango wa kutafuta taarifa ya mwitikio wao katika yale tuliyowatia moyo kuyafanyia matengenezo ifikapo siku ya sabato

Makusudi ya program hii ni kuongeza idadi ya watu watakao iunga mkono bajeti ya kanisa ma maidara katika kukamilisha utume wake. Jambo la msingi kukumbukwa hapa ni kwamba si kazi ya wanamatembezi kuwaelekeza waumini kiasi wanachotakiwa kutoa. Lengo si kiasi cha pesa, lakini lengo ni asilimia 100 ya washiriki wanaojisikia kushiriki katika utume wa kanisa. Kiasi atakachotoa mtu ni kazi ya Roho Mtakatifu na mtu mwenyewe.

Kamati ya matembezi inaweza kuwajulisha tu waumini kiasi ambacho kanisa linahitaji kwa kila mwezi, lakini haipaswi hata kidogo kujaribu kumwambia mtu kiasi gani atoe. Wanaweza kumwachia kadi itakayojazwa kwa hiyari yake na hawapaswi mtu kuiulizia katika matembezi, bali watasubiri mpaka atakapoileta mwenyewe kanisani.

Mualike mtu au familia kuyatambua mapenzi ya Mungu kwao, kwa njia ya kuwaombea, kaini pia watolee wito wa kutumia, muda, ujuzi na mapato pia kwa Mungu wao. Maombezi yatakua ndio mwisho wa program ya matembezi hapo nyumbani wakati wanatimu watakapokua wakitoka. Ikia program hii itafanyika kwa uzuri kabisa itakua msaada mkubwa katika kukuza idadi ya watu watakaoiunga mkono bajeti ya kanisa na kuleta mwitikio mzuri katika utoaji.

Kwa kawaida wale wajumbe wa baraza na timu ya nyumba kwa nyumba hufanya maamuzi ya kujitoa katika mambo ya uwakili kabla ya kuwaendea watu majumbani mwao.

## Aina za Watoaji Kanisani

Kiwango cha waaminifu kinaweza kuongezeka kwa kutambua na kuwafikia watu ambao wanakua katika makundi ya watu wafuatao:

***Watu wa kulifurahia kanisa.***

Kwa bahati mbaya sana, katika makanisa yaliyomengi kuna asilimia kadhaa za washiriki ambao hawatoi chochote kuungana na kanisa zima katika kuufikia utume wa kanisa la Mungu. Hawa watu hufurahia faida na fursa za ushirika, lakini mara nyingi hawaoni wajibu wowote walionao. Wengine hawaoni utume wa kanisa lao, au wengine wamepoteza imani juu na namna kanisa linavyotumia matoleo yanayopatikana. Baadhi ya waumini hawana au wamepata elimu ndogo juu ya uwakili na matumizi binafsi ya mali waliyonayo.

***Watu wa matukio:***

Mara nyingi watu hawa hawana mahudhurio mazuri kanisani – huenda wengine mara moja tu kwa mwezi, au wakati mwingine mara tatu au mara nne kwa mwaka mzima. Mara nyingi matoleo yao huwa katika kiwango kile kile cha siku zote.

***Watu wa miradi:***

Idadi inayoongeza katika matoleo ni ile ya watu wanaotoa kwa matukio. Wanaunga tu mkono miradi ya kanisa ambao inawavutia. Ni lazima kwanza pawe na mradi mkubwa au kazi maalum ya kufanyika ili waweze kutoa sadaka zao.

***Watu wa msisimuko:***

Hawa ni watu wanaohudhiria sana kanisani lakini huwa na maamuzi ya utoaji kwa vipindi maalum na kisha kujisahau tena au kuacha kujali maamuzi waliyoyafanya. Wenyewe huwa na utaratibu wa kutoa katika vipindi vipindi, lakini utoaji wao si ule wa kudumu.

***Watu wanaotoa kwa mpango:***

Wastani wa asilimia 25 kati ya washiriki walio makanisani, ni wale ambao wanatoa kwa uaminifu. Hawa ni watu ambao wahudhuria ibaka kwa umakini mzuri na hushiriki katika huduma mbalimbali za kuutimiza utume wa kanisa. Baadhi ya washiriki ambao wako katika kundi hili huwa na kawaida ya kukua katika matoleo

## Njia za kuongeza matoleo

**Watembelee mara kwa mara washiriki wapya majumbani mwao. Waalike katika familia ya kanisa lao na jitolee kujibu maswali yoyote yale waliyonayo juu ya matumizi ya matoleo kanisani.**

**Waeleze watu jinsi Mungu alivyokubariki wewe binafsi katika mapato yako pale ulipokua mwaminifu.**

**Toa bahasha kwa watoto na vijana na watu wazima katika shule ya sabato asubuhi. Elezea jinsi ya kuzijaza na zungumzia umuhimu wa kutoa zaka na sadaka.**

**Andaa program ya washiriki kutoa ushuhuda (dakika 3 – 4) binafsi sabato asubuhi. Wanatakiwa kujiandaa vizuri na wawe na ujumbe unaojenga wa namna walivyoanza kutoa matoleo, jinsi Mungu alivyowabariki, na jinsi wanavyokusudia kukua katika matoleo na uaminifu.**

**Jifunze kwa makini sana juu ya matumizi mazuri ya zaka na sadaka, tangu kuzihesabu hata uandishi wa risiti na mpaka taarifa ya muhazini. Ikiwa kutakua na hitaji, toa mapendekezo juu ya ufanisi, uwajibikaji, na kutunza siri za matoleo ya washiriki.**

**Toa taarifa za matoleo mara kwa mara. Maendeleo ya matoleo ya kanisa yatolewe mara kwa mara pia, tumia vipeperushi kanisani, matembezi ya nyumba kwa nyumba au mbao za matangazo, na hata taarifa za mdomo.**

**Simamia kwa umakini sana masomo yanayotolewa wakati wa ibada ya matoleo. Yawe ni masomo yaliyoandaliwa vizuri na yenye msisitizo na mguso wa uaminifu. Mtoaji wa somo ajiandae vizuri.**

**Vyombo vya matoleo vinatakiwa kuwa katika mfumo wa sanduku ambalo linawekwa mbele kanisani ili kila mtu aongozwe na shemasi zamu kwa zamu, katika kuleta matoleo yake pale mbele kwenye sanduku. Sanduku lisiishie kuwa kubwa tu bali liwe zuri na linalovutia sana.**

**Kuwe na program ya kutoa asilimia ya vitu kama vile mifugo, mazao mashambani, n.k.**

## Matumizi ya Pesa Yanayomtukuza Mungu

Wakristo Waadventista wanaamini kwamba Mungu amewapatia wanadamu umiliki wenye masharti. Tunakubali kwamba Mungu ndiye Muumbaji na kwa sababu hiyo mmiliki wa kweli wa ulimwengu wote na vyote vilivyomo. Jambo muhimu katika matumizi mazuri ya pesa ni kwamba pesa na hata mali nyingine lazima vitumike kwa mapenzi na maelekezo ya mwenye navyo.

Hatutakiwi kusashau kwamba tumewekwa katika dunia hii kwa majaribio, kuona kwamba tunaweza kufaa kuishi katika maisha yajayo. Hakuna mtu aliyepumbazwa na ubinafsi wa ulimwengu huu atakayeingia mbinguni. Kwa hiyo Mungu anatupima hapa, kwa kutupatia vitu tuvimiliki kwa muda kitambo kwanza, ili kwamba matumizi yetu yaonyeshe kwamba tunaweza kuaminika kupewa utajiri wa milele. (*Counsels on Stewardship*, p. 22).

Kwa kuwa umiliki wetu wa pesa na mali ni kipimo cha hatima ya umilele wetu, kila mkristo anahitaji kujua masharti na kanuni za Mungu zinayopaswa kufuatwa katika matumizi.

. **Mapato ya pesa**. "kwa jasho la uso wako utakula chakula..." (Mwanzo 3:19). Baada ya Adam na Eva kuondoka Edeni mwanadamu alitakiwa kuishi kwa kufanya kazi. Hebu chunguza nuru hii kutoka kitabu cha Pambano Kuu: Hakuna jambo linaloharibu mwenendo au jambo la hatari sana, hasa kwa vijana, kama kupata pesa au mali pasipo kufanya kazi." (uk. 387) ni lazim tuchague kuikataa nadharia ya ulimwengu huu (ambayo hufundisha kupata mali nyingi inavyowezekana, haraka sana inavyowezekana, kwa njia yoyote inayowezekana). Tunatakiwa kukubaliana na mfumo wa upatikanaji pesa na mali unaoendana na maagizo ya maagizo ya Mungu.

. **Rudisha zaka**. Kinyume kabisa na imani iliyoenea sana, kanuni ya urejeshaji wa zaka haikuwekwa kwa ajkusudi la kuwaungamkono watumishi makanisani. Hayo ni matumizi tu mojawapo ya pesa kwa jinsi ya maagizo ya Mungu. Sababu ya kutoa zaka ni kuonyesha uaminifu kwa Mungu na kumtambua kama mmiliki wa kila kitu. Hili linaonekana kwa mara ya kwanza pale Edeni kupitia katazo la mti mmoja tu wa ujuzi wa mema na mabaya. Mti huu ulikua ni ukumbusho wa kudumu kwamba Mungu ndiye mmiliki wa kila kitu hapa duniani. Mungu alikua amewazuia Adam na Eva lakini walishindwa kuitunza kanuni hii ya uwakili (*Testimonies*, vol. 6, p. 386.) utoaji wa zaka ni jambo la kudumu linalotukumbusha kwamba Mungu ndiye mmilikiwa kila kitu duniani hapa.

"'Leteni zaka kamili ghalani, ili kiwemo chakula katika nyumba yangu, mkanijaribu kwa njia hiyo, asema Bwana wa majeshi; mjue kama sitawafungulia madirisha ya mbinguni, na kuwamwagieni baraka, hata isiwepo nafasi ya kutosha, au la." (Malachi 3:10).

Kabla kiasi chochote cha pesa hakijatumika, kwanza umtambue Mungu kama mmiliki kwa kutenga pembeni kile ambacho Mungu amekihitaji. Hili si jambo la kuonyesha shukrani au ukarimu, lakini ni jambo linaloonyesha uaminifu na utii wako kwa Mungu. Wote wanaofuata kanuni hii kwa umakini watagundua kwamba: kupitia mibaraka anayotoa Mungu ile asilimia tisa inayosalia pamoja na mibaraka ya Mungu, inatosha kabisa kuliko kumi ya kumi ambayo haina mbaraka wa Mungu.

. **Toa sadaka**. "Kila mtu na atoe kama awezavyo, kwa kadiri ya baraka ya Bwana, Mungu wako, alivyokupa." (Kumb. 16:17). Utoaji wa sadaka ni njia ya kuonyesha upendo na shukrani kwa Mungu, inayotolewa na mtu mwenye hiyari kwa jinsi Mungu anavyodumisha maisha yake, anavyostahili kuabudiwa na kwa jinsi kazi ya Mungu unavyodhihirika. Wote ambao hutoa sadaka watagundua thamani ya kujitoa kwa manufaa ya watu wengine.

**Kwa kawaida sadaka hugawanyika katika maeneo makuu manne:**

Kanisa mahalia (50%)
Sadaka ya Konferensi (20%)
Utume ulimwenguni kote (20%)
Miradi maalum (10%)

Washiriki wanaombwa kuielekeza sadaka yao ktk malengo haya makubwa manne. Haya maeneo makubwa manne yanatakiwa kuonyeshwa katika bahasha za matoleo ya zaka na sadaka kwa mujibu wa Sera ya kanisa. (see General Conference Working Policy, Sec. T 05).

- **Kuweka akiba**. Wakristo wanatakiwa kuendeleza tabia ya kuweka akiba maishani mwao kwa kila pato, hili ni jambo la muhimu sana katika kuwa na matumizi bora ya pesa kwa kuwa itakusaidia katika mambo yaliyokua katika mpango na hata katika mambo yanayoibuka kama dharula. Lakini hata hivyo, ipo tofauti, kati ya kuweka akiba na kulimbikiza pesa pasipo matumizi yanakusudiwa. Mungu atawabariki wale ambao huweka pesa kwa lengo la akiba. Kwa upande mwignine, pesa iliyowekwa bila kusudi lolote lile ni hazina iliyozikwa.

- **Epuka madeni**. Kuna uwezekano mkubwa kwamba mbraka mkubwa na faida ya kuweka akiba ni kuwasaidia watu kuepuka kuingia katika tatizo kubwa la kuishi kwa madeni hasa inapotokea dharula ya jambo flani. Kuna mazingira flani flani ambayo mtu analazimika kuingia katika deni. Hata hivyo mtu hapaswi kuingia katika deni pasipo kuwa na mkakati wa jinsi ya kulilipa deni hilo. Madeni mengi yanayozitesa familia nyingi leo hii yanatokana na sababu hizi kuu mbili: kushindwa kuishi kwa bajeti na kushindwa kutofautisha kati ya matakwa na mahitaji.

  Ni lazima tukumbuke kwamba Katika Mathayo 6:31-33 Yesu hakumuomba baba atupatie matakwa yetu – alitufundisha kuomba mahitaji yetu. Elimu ya uwakili inaweza kumsaidia mtu kuwa na ukomavu katika namna ya matumizi sahihi ya ya pesa na kumsaidia mtu kuona tofauti iliyopo kati ya mahitaji na matakwa.

- **Wekeza**. Wale wote ambao wamepata mali kwa njia yenye uadilifu, wanaweza kutumia busara kwa mpango makini, kuwekeza ili kwa ukarimu wao kazi ya Mungu itiwe nguvu. Ndipo baadaye mkristo mwaminifu atasikia sauti ikisema:
  Bwana wake akamwambia, Vema, mtumwa mwema na mwaminifu; ulikuwa mwaminifu kwa machache, nitakuweka juu ya mengi; ingia katika furaha ya bwana wako! (Mathayo 25:23)

***Uwakili ni picha ya upande wa mahusiano kati ya mwanadamu na Yesu, unaoonyesha jinsi mwanadamu anavyoshiriki kudumisha mahusiano hayo.***

Mtuanapaswa kwanza kuishi katika uzoefu wa injili, kabla hawajawa wakili bora wa Kristo

## Maelezo ya Idara ya Uwakili

### Utangulizi

Mara nyingi watu wamedhani idara hii ni kwa ajili ya ukusanyaji wa pesa, kwa kweli huduma ya idara ya uwakili ipo ili iwasaidie waumini kuwa wanafunzi wa Kristo katika matumizi ya mali ambazo Mungu amewapatia wanadam. Hii inahusika na matumizi ya maiili yetu, vitu tunavyomiliki, uwezo (karama) na hata muda pia.

Yesu alitumia muda wake mwingi akizungumzia juu ya vitu/mali ambazo mwanadamu huwa nazo. Alijua kwamba wasikilizaji wake wasingeliweza kuelewa vizuri kanuni za ufalme wa Mungu, mpaka kwanza wameelewa mahusiano yao ya kiuwakili na Mungu wao. Aliwaambia makutano katika hubiri lake la pale mlimani kwamba, "kwa kuwa hazina yako ilipo, ndipo utakapokuwapo na moyo wako." (Mathayo 6:21).

Mungu analiuliza kanisa kuwa jumuiya ya wanadmu wenye lengo moja la kila mmoja kumtunza mwenzake kiroho, wanapokua hatua kwa hatua katika imani. Agano jipya huliita kanisa "mwili" (Waefeso 1:22)

Kristo anatuita katika mwili Wake kwa kusudi la kudumisha uhusiano wa wokovu kati yetu sisi na Yeye, na miongoni mwa wanajamii ya waumini. Ellen White anasema, "Kila muumini anatakiwa kujitoa kwa moyo wote kwa jinsi anavyojitegemeza kwa kanisa. Mafanikio ya kanisa yanapaswa kuwa jambo la kwanza kwa kila mtu. Ni jambo ambalo liko katika uwezo wa kila mmoja kufanya jambo flani kwa ajili ya Mungu wetu. (Counsels on Stewardship, page 42).

Kanisa linakua ni uzoefu, ambapo kila mmoja wetu anajifunza. Washiriki wanatakiwa "kutiana moyo kuonyesha upendo na matendo mema" na "kuachana na hali ya kutojumika pamoja, bali wadumishe kutiana moyo kila mmoja na mwenzake." Katika kukua kwa mkristo (Waebrania 10:24 - 25). Hii nidyo njia ambayo kila mmoja anaonyesha kumjali mshiriki mwenzake na kumuhudumia mwenzake.

Karani wa uwakili katika kanisa mahalia au mwenye kiti wa kamati ya fedha, kama kiongozi mwingine yeyote wa kanisa, naye pia ni mtumishi kanisani. Kila mshiriki anaitwa katika huduma, akiwa na karama flani za Roho Mtakatifu, na hata kupitia ubatizo tunakumbushwa kwamba tunapewa utume na kupokea agizo.

Mungu humpatia kila muumini kanisani vitu flani kwa ajili ya huduma - maandiko matakatifu, uwezo wa maisha ya kiroho, tabia ya Mungu, na karama za roho.
Kutambua kwetu kwamba Mungu ndiye mmiliki wa vyote hutuongoza katika uaminifu wa matumizi mazuri ya vitu tulivyopewa kwa utukufu wa Mungu. Huu uaminifu unapimwa kwa jinsi tunavyorejesha zaka na sadaka za kumtukuza Mungu kwa uaminifu wake na jinsi anavyotupatia uhai.

# Kazi za kiongozi wa uwakili kanisani

Idara hii ambayo mtu anaitwa kusimamia katika kanisa, inaweza kuelezeka kwa maneno machache kwa namna ifuatayo:

1. Elimu ya uwakili. Kuwafundisha washiriki juu ya kanuni bora za uwakili kanisani, ni jambo la muhimu kabisa katika wajibu alionao katibu wa uwakili. Hii inahusika na kuandaa na kusimamia program ya semina za uwakili, kumsaidia mchungaji kupangilia madarasa ya kujifunza masomo ya uwakili, kuweka utaratibu mzuri wa matoleo ya zaka na sadaka katika ibada na kufunsisha juu ya shana ya uwakili katika shule ya sabato au wakati mwingine unaofaa kujifunza. Pia huwasaidia washiriki wapya kuelewa juu ya kanuni za kiuwakili katika maisha ya Wakristo.
2. Kuweka mipango na bajeti. Kama mjumbe wa baraza la kanisa, katibu wa uwakili anatakiwa kujua hatua kamili za uwekaji mipango kanisani, na kusaidia katika kuweka mikakati ya ukusanyaji wa matoleeo kwa ajili ya utume wa kanisa. Anaweza kuwa mwenyekiti au mjumbe katika kamati ya mipango na bajeti ya kanisa. Inashauriwa na kutakiwa kwamba mpango kazi na bajeti ya kanisa viende pamoja na visiwe vitu viwili tofauti.
3. Vikao vya kamati ya fedha. Japo katika makanisa madogo inashauriwa katibu wa uwakili awe mwenyekiti wa kamati hii, haitakua na ubaya ikiwa atakua mjumbe wa kamati hii.
4. Kutembelea washiriki. kiongozi wa uwakili ndiye ambaye kwa kawaida anapaswa kusimamia program ya kutembelea mshiriki mmoja mmoja akisaidiwa na timu ya watu wanaotembelea. Hawa watashirikiana kupanga nani atembelewe kwa wakati flani na kwa kusudi gani mtu atembelewe katika matembezi hayo.
5. Kukazia teolojia ya zaka na teolojia ya sadaka. Washiriki walio wengi hawana ufahamu wa kutosha juu ya elimu ya msingi wa kiteolojia wa ibada ya uwakili wa matoleo. Watu walio wengi hutoa tu zaka na kuzuia sadaka kwa kuwa hawajui teolojia au msingi wa kimaandiko wa matoleo ya sadaka. Kutoa elimu hii kutasaidia kuongeza uelewa wa matoleo hayo katika ibada zetu.
6. Kuhimiza kwa uongozi wa kanisa juu ya kutoa taarifa za mara kwa mara za maendeleo ya matoleo kwa washiriki. Waumini wapate taarifa za matoleo waliyofanya kila mwezi kwa kadri inavyowezekana.
7. Washiriki wanaotoa wapongezwe kwa kutembelewa na mchungaji au kutumiwa ujumbe wa maandishi moja kwa moja kutoka kwa mchungaji wa kanisa husika. Mkuu wa uwakili amkumbushe mchungaji na ashirikiane naye kuwatambua wale wanaotoa kwa mpango.


Uwezo
Mwili
Talanta
Mali
Fedha
Muda